LEGAL AND HUMAN RIGHTS

LEGAL AID UNIT - BUGURUNI

P.O. BOX 79643, DAR ES SALAAM, TANZANIA
Tel: 2862794 Dar es salaam

LHRC/LAC/BGN/05/305/02 **DATE:** 20 May 2005.

KURUTHUMU JABIRI
TANZANIA TELECOMMUNICATION COMPANY LIMITED, EXTELECOMS HOUSE 6TH FLOOR HQ,
DAR ES SALAAM,

K.K. MANAGER BILLING,
TANZANIA TELECOMUNICATION COMPANY LIMITED,
EXTELECOMS HOUSE 6TH FLOOR HQ,
DAR ES SALAAM

YAH: NIA YA KUSHITAKI

Rejea kichwa cha somo hapo juu

Tumempokea Ndugu aitwaye Margareth Kamgwawa katika ofisi zetu zinazotoa msaada wa kisheria zilizopo Buguruni. Hivyo Ndugu Margareth Kamgwawa sasa ni mteja wetu anayepata msaada wa kisheria katika kituo chetu cha msaada wa sheria hapa Buguruni.

Ndugu huyu ametueleza yafuatayo:

1. Kwamba anaye mume wake wa ndoa aitwaye Ndugu **MOSES KAMGWAWA** ambaye wameishi naye kwa muda wa miaka 21.

Board of Directors
Bishop Elinaza Sendoro (Chairman), Dr. R.W. Tenga, Ananilea Nkya, Dr. Sengondo Mvungi, Martin Saning'o,
Azaria Mbughuni, Rose Camil, Dr. Palamagamba Kabudi

2. Kwamba wamejaliwa watoto 3 katika ndoa yao ambao ni:
    1. Ruth Moses Kamgwawa,miaka 20.
    2. Geoffrey Moses Kamgwawa, miaka 19.
    3. Gloria Moses Kamgwawa, miak 13.

3. Kwamba wameishi kwa amani na upendo na kushirikiana na mume wake huyo kwa muda wote huo mpaka ilipofikia mwaka 2003 mwezi wa tatu alipogundua kuwa wewe unao uhusiano wa mapenzi na mume wake.

4. Kwamba baada ya kugundua hilo alinyamaza hakutaka ugomvi, lakini cha kushangaza ni pale ulipofikia hatua ya kuingia mpaka ndani ya nyumba anayoishi iliyopo Kinyerezi siku ya Alhamisi 05/05/2005 majira ya saa 3:00 asubuhi bila ya idhini yake kitendo ambacho kinaonyesha kuwa baada ya kumchukua mume wake unataka mpaka kuingia ndani nyumba yake ya ndoa.

5. Kwamba licha ya huo uhusiano amegundua pia kuwa unakaa na mume wake nyumbani kwako Segerea tangu 2003 mapaka tunapoandika barua hii.

6. Kwamba kutokana kuishi huko na mume wake, anashidwa kupata matunzo ya mume wake na pia anashindwa kupata haki ya ndoa kama mke.

7. Kwamba hali hii imesababisha watoto wake pia kukosa matunzo kutoka kwa baba yao na kumfanya mteja wetu kuhangaika na watoto.

8. Kwamba kutokana na maelezo yote hayo mteja wetu ametuagiza kukuandukia waraka huu wa kisheria ili uweze kuachana na mume wake mara moja, mara upatapo barua hii. Na pia uweze kumlipa fidia ya mateso uliyompa jumla ya shilingi milioni ishirini

fedha za kitanzania(20,000,000/=) ndani ya siku 21 kuanzia siku utakayopata waraka huu.

Chukua tahadhari kuwa huu ni waraka halisi wa kisheria na mteja wetu anahitaji utekelezaji wa maombi yaliyomo ndani ya barua hii ndani ya siku 21. Kinyume cha hayo tutamshauri mteja wetu kufungua kesi ya madai mahakamani kwa gharama zako binafsi.

Tunatanguliza shukurani zetu za dhati,
Wako,
KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU,

DOROTHY PHILIP.
K.N.Y. MKURUGENZI MTENDAJI.